

KILE MUNGU ALICHO AHIDI KATIKA SIKU HII YA LEO

Inategemea unaangalia nini. Kama unaangalia kule kutimia kwa ahadi ya leo, utaiona; lakini kama unaangalia hekima fulani ya kibinadamu, au kitu fulani ambacho siku zote wamekuwa wakikiangalia – mwanzilishi mkubwa, Mwana historia, mtu mwingine awaye, kitu kingine – hutaweza kuiona. Lakini unapomwangalia yeye kupitia Neno, Neno linamtangaza yeye kuwa ni nani [1]

Baadhi ya ahadi za siku hii ya leo ni:

1) KUOLEWA KWA BIBI ARUSI (Ufunuo 19:6-10)

- Mkewe Amejiweka Tayari-

Sasa- kumbuka, yule hakuwa ni Yesu akizungumza na Ibrahimu pale. Ambaye aliweza kupambanua mawazo yaliyo katika nia ya Sarah nyuma yake. Huyu hakuwa ni Yesu; alikuwa bado hajazaliwa. Lakini ilikuwa ni mtu katika umbo la kibinadamu, ambaye Ibrahimu alimwita “Elohim, Yule Mkuu Mwenyezi” (Mwanzo 18:1-18), akionyesha.....”Na Yesu alisema kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma”, Sasa angali kwa karibu, katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa wakati wa kuja kwake Mwana wa Adamu, wakati Mwana wa Adamu atakapofunuliwa” (Luka 17:26-30). Siyo tena kama Kanisa, siyo tena; Bibi Arusi amekwisha kuitwa “Katika siku ile mwana wa Adamu atakapofunuliwa “ Ni nini kuliunganisha Kanisa katika kichwa, kuunganisha, kuolewa kwa Bibi Arusi.

Ule mwito wa Bwana Arusi utakuja hasa kupitia hii, wakati Mwana wa Adamu atakapokuja chini na kuja katika mwili wa kibinadamu kuwaunganisha hawa wawili pamoja. Kanisa inabidi liwe ni Neno; yeye ni Neno, na hawa wawili wanaungana pamoja, na ili kufanya hivyo, itachukuwa udhihirisho wa kumfunua Mwana wa Adamu. Siyo kiongozi wa dini. sijuiunaona nilichomaanisha?

Unaona, ni Mwana wa Adamu, Yesu Kristo, atashuka chini katika umbo la kibinadamu kati yetu, na atalifanya Neno lake halisi kiasi kwamba italiunganisha kanisa na Yeye kama kitu kimoja, Bibi Arusi, na halafu atakwenda nyumbani kwenye karamu ya Arusi Amen. Tayari ameunganika; tunaenda kwenye karamu ya Arusi. Neno hapa linapoungana na mtu, na hawa wawili wanakuwa mmoja, na halafu linafanya nini tena? Linamdhihirisha mwana wa Adamu tena, siyo kanisa la watheolojia, yule Mwana wa Adamu. Neno na kanisa **VINAKUWA MMOJA**. Vyovyote Mwana wa Adamu anavyotenda, Alikuwa Neno, Kanisa linafanya jambo hilo hilo. [2]

2) MWANA WA ADAMU AMERUDI TENA KANISANI

akifunuliwa ndani ya mwanadamu, siyo Mwana wa Mungu kwanini Mwana wa Adamu tena amerudi kanisani mwake tena akatika siku za mwisho. Tunaona ameahidi hilo katika Ahadi za Mungu.

Na tunaona kwamba Mungu siku zote amejifunika ngozi Musa alipomuona yeye, Alikuwa amejifunika ngozi juu yake; Alionekana kama Mwanadamu (Kutoka 33:12-23) Mungu alipokuwa nyuma ya pazia, Alikuwa na ngozi juu yake. Na Mungu usiku wa leo katika kanisa lake amefunikwa ndani ya kanisa lake na ngozi juu yake. Ni Mungu yule yule usiku wa leo. Tunaona hilo.

Lakini sasa, kama ilivyo, lile pazia la ngozi ndilo linalowanasa katika mapokeo. Hawawezi kuamini tu kuwa ni Mungu anayewafanya wafanye kama hivyo, Unaona? Ni kwa sababu Mungu amefunikwa, katika kanisa lake na ngozi juu yake hiyo ni kweli. Amefunikwa mbali na asiyeamini na anafunuliwa kwa anayeamini ndiyo bwana. Sasa, wakati pazia la kawaida zao za wazee na Neno likawekwa wazi (oh kwa hakika leo), hapo sasa linaweza kuonekana dhahiri, tunamuona yeye Mungu tena akiwa amefunikwa katika ngozi ya kibinadamu. Waebrania 1 ilisema hivyo, na tena mwanzo 18. Unakumbuka Mungu alikuwa ni mtu, akiwa amesimama pale akila na kuzungumza na Ibrahimu, na kumuambia kile Sara alichokuwa akifanya nyuma ya hema. Na Yesu alisema, “kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa wakati wa kuja kwake Mwana wa Adamu” Uungu ukiwa umefunikwa tena katika mwili wa kibinadamu. Sasa kumbuka, Yesu hakusema, wakati Mwana wa

Mungu akiwa anafunuliwa” katika Luka sura ya 17, Ninaamini, na kama mstari

wa 30; Alisema na wakati Mwana wa Adamu atakapofunuliwa” Mwana wa Adamu akiwa amerudi katika kanisa, akifunuliwa ndani ya wanadamu, siyo Mwana wa Mungu, lakini Mwana wa Adamu tena, akiwa amerudi ndani ya kanisa tena katika siku za mwisho. Tunaona hilo Aliahidi hilo katika Ahadi za Mungu.

Tunaona kitu kingine katika Agano la kale (nina maandiko hapa katika kutoka) kwamba zile ngozi za zamani za pomboo (kutoka 26:14) Ilifanya nini? Iliuficha utukufu wa Mungu kutoka kwa watu: ngozi za pomboo. Sababu watu hawakuweza kuliona hilo, ni kwa sababu lilishikiliwa kwenye ngozi..... Utukufu wa Mungu ulikuwa nyuma ya ngozi na sasa, utukufu wa Mungu uko nyuma ya ngozi yake (Hiyo ni kweli), na kanuni haziwezi kuliona hilo ilikuwa ndani ya pazia mahali Neno lake lilikuwa [3]

Mwana wa Adamu ni Kristo, Ni yeye ambaye mnamla. Hamumli mtu, mtu maneno yake yanashindwa, lakini manakula kile kisichoshindwa mwili – Neno la Mwana wa Adamu [4] (Luka 17:28-36; Joel 2:28)

(3) Na sasa, ROHO MTAKATIFU KWA UTIMILIFU WOTE ANALITEMBELEA KANISA

Akimfanya Mungu katika mwili wa kibinadamu kama alivyofanya kabla ya Sodoma kuteketezwa pale, ambayo ilikuwa ni mfano [5]

Roho Mtakatifu alikuwa amefungwa na mito hii ya kidhehebu, kwa karibuni miaka elfu mbili, lakini atafunguliwa wakati wa jioni, kwa ujumbe wa wakati wa jioni. Roho Mtakatifu akiwa amerudi tena katika kanisa; Kristo, mwenyewe akifunuliwa katika mwili wa kibinadamu, wakati wa jioni. Alisema aliahidi hilo [6]

(4) HUKU NDIKO KULE KUJA KATIKA MVUTO WA TATU Lakini haitakuwa ni kitu cha kuonyesha hadharani [7]

Hakutakuwa na uigizaji kama ilivyokuwa katika ile mivuto miwili (ambayo ilikuwa ni uponyaji na kutoa unabii) Na tunaangalia, Bwana ule Mvuto wa Tatu ambao tunajua kwamba utafanya mambo makubwa

kwa ajili yetu miongoni mwetu [8] utakuwa kwa hakika kwa wale waliopotea kabisa, lakini utakuwa kwa Bibi arusi na kanisa [9]

Lakini uliona, ile ilitolewa kwa kupenda kwake mwenyewe sijamwomba yeye kamwe, Bwana, nipe mimi nifanye hiki, kunena na vitu vile vikawepo kama vile, kufanya mambo hayo pale” Kamwe sijamwomba yeye hilo. Yeye kwa mapenzi yake ya kimungu alikuja kwangu na kusema “Nenda ukafanye hivi” Sikuwa nimeomba kitu chochote juu ya hilo [10]

(5) TUNAKUJA SASA KWENYE UKAMILIFU, kwa sababu inabidi watu waje kenye hili ili unyakuo uweze kutokea. Hilo ndilo linalozuia huo usifanyike sasa, unasubiri kanisa lije katika ile Imani kamilifu ya kunyakuliwa. Ni mahali pakamilifu (2 Kor 5:1-8; Yohana 14:1-3), pakikuita wewe kwenye ukamilifu na inabidi uwe makamilifu ili ufike pale. Biblia ilisema hivyo Yesu alisema, Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu. (Matayo 5:48; Waebrania 10:14)

Siyo imani, lakini imani kamilifu iliyojengwa hapa juu. Na angalia Mungu mkamilifu, akiwa na moyo mkamilifu, akishika ahadi kamilifu, kwa Neno lake kamilifu [11] Wale walioishi nyuma pale hawakuwa wakamilifu mpaka hili kanisa likamilishwe, kundi la Bibi Arusi katika siku za mwisho kuwaleta wote ndani na wote pamoja wachukuliwe juu (Waebrania 11:39-40) Na leo, tunayo, kwa msaada wa Mungu tafsiri kamilifu ya Neno iliyothibitishwa na Mungu [12] (I Kor 13:9-10)

(6) MVUA YA MWISHO KUMWAGWA JUU YA WATU KATIKA SIKU ZA MWISHO (Yoeli 2:28-32) Nafikiri Neno la kigiriki hapa ni “Kenos” ambalo linamaanisha kuwa “Alijimwaga mwenyewe nje” siyo katika njia ambayo tungenesema, kama kitu kilikuwa ndani ya kingine kitolewe nje, lakini alijimwaga mwenyewe nje. Alijibadilisha yeye ni “en Morphe”

Alijibadilisha kutoka kile alichokuwa kuja kwa alichosasa kamwe habadili asili yake [13].

Hiyo ni kuwa, alijibadilisha mwenyewe; “Alijimwaga Mwenyewe” kuwa ndani ya kufuniko, kuwa katika umbile lingine; siyo mtu mwingine aliyetoka kwake aitwaye Roho Mtakatifu, Lakini ilikuwa ni

yeye mwenyewe. Unalipata hilo? Yeye mwenyewe alijimwaga mwenyewe ndani ya watu: Kristo ndani yako (Wakolosai 1:26-27) jinsi ilivyo ya kupendeza ilivyo ya ajabu kufukiri. Mungu akijimwaga mwenyewe ndani ya mwanadamu, na kuwa ndani ya mwaminio: kujimwaga ilikuwa ni sehemu ya mchezo wake kufanya hivyo. Mungu kwa utimilifu wote, Uungu wote kwa jinsi ya mwili ulikuwa katika utu wa Yesu Kristo (Kolosai 2:9) Alikuwa ni Mungu na Mungu pekee, siyo nafsi ya tatu au nafsi ya pili au nafsi ya kwanza: Lakini yule nafsi, Mungu akifunikwa katika mwili wa mwanadamu [14] (Yohana 5:20) Oh, kutakuwa na mvua za kweli za kwanza (masika) na mvua za mwisho (vuli) katika siku za mwisho kwa lile kundi dogo ambalo linakuja Naye katika punda huyu mdogo, mpole na mnyenyekevu, hakuna shaka au dhehebu, wakipiga kelele (kulia) “Hosiana kwa mfalme ambaye anakuja kwa jina la Bwana” kuna nini leo? Nini kinavutia pale mlimani? [15]

(7) “WAKATI WA JIONI, ITAKUWAKO NURU”, Alisema (Zakaria 14:7) na mwana yule yule liyejimwaga nje mwenyewe “Kenos”. Siku ile ya pentekoste, aliahidi kufanya jambo lile lile wakati wa jioni. Ni sawa na ahadi [13] (Zaburi 119:105; Yohana 8:12)

(8) NI WAKATI WA KUUNGANIKA KWA MUNGU NA BIBI ARUSI WAKE. Kristo, aliyekichwa cha kweli akija katika Bibi Arusi wake, akifanya kazi zile zile alizozifanya pale Mwanzoni (Yohana 14:12) Ule mwili na kichwa vinakuwa mmoja katika Matendo na katika ishara na katika maisha, Vikithibitishwa na Mungu Mwenyewe kupitia Neno lake lililoahidiwa la siku za mwisho. Aliahidi hili katika siku, siku za mwisho. Sasa, kama wewe ni wa kiroho utalinasa hilo kile kichwa na mwili vimekuwa kitu kimoja. Ni Mungu akidhihirishwa ndani ya watu wake. Hiyo ndiyo sababu Mume na mke siyo wawili tena; bali ni mmoja. Mungu na kanisa lake ni mmoja. Kristo ndani yako, ufunuo mkuu wa Mungu hata anaitwa kwa jina lake. [16] Unaona makanisa yanaungana, mataifa yanaungana, lakini ni wakati wa Mungu kuunganika na Bibi Arusi wake pia [17]

(9) NGUVU ZINAZOENDESHA ZA KANISA HILI ITAKUWA NI KUJAZWA UPYA NA ROHO MTAKATIFU, kwamba tumetenda katika kiwango kidogo, wakati lile jiwe la kifuniko linakuja

chini kuungana na mwili lakini pale mwili na kichwa vinapoungana pamoja nguvu kamili ya Roho Mtakatifu itamwinua Bibi Arusi juu hasa kama vile..... Nguvu za kuendesha ni Roho Mtakatifu [17]

Kutakuwa na uvumi kutoka mbinguni ambao utachukuwa ubatizo wa Roho Mtakatifu ndani ya Bibi Arusi ambao utamchukuwa yeye (Bibi Arusi) kutoka duniani kuingia katika Neema ya kunyakuliwa kwenda utukufuni katika unyakuo. Mungu aliahidi hilo [18] (1 Wathesa 4:13-17; 1 Petro 1:3-5).

(10) LILE NENO LIMETIKISWA TENA MIONGONI MWA WATU,

kwamba kanuni mfu za watu zimekufa na Mwana wa Mungu anaishi tena na ubatizo wa Roho Mtakatifu ukiwa hasa miongoni mwetu na unatupa sisi uzima [19] (Walawi 23:9-11)

(11) ZILE SIRI ZA NGURUMO SABA ZIMEFUNULIWA kupitia kule kufunuliwa kwa mihuri saba (ufunuo 10:1-7) ili kumleta Bibi Arusi pamoja kwa ajili ya Imani ya kunyakuliwa na kutupa imani kwa ajili ya neema ya kunyakuliwa kwa ajili ya kanisa kuondoka [20]

Sasa huyu mjumbe wa malaki 4 na ufunuo 10:7 anaenda kufanya mambo mawili moja kutokana na malaki 4 ataigeuza mioyo ya watoto iwaelekee baba zao pili: Atafunua siri ya zile ngurumo saba za ufunuo 10 ambazo ni funuo zilizo kwenye mihuri sabab. Itakuwa ni hizi kweli za siri zikifunuliwa kiungu ambazo zinageuza mioyo ya watoto kuwaelekea mababa wa Pentecoste (Mitume) Hasa iko hivyo [21].

(12) ROHO YA HEKIMA na ufunuo katika kumjua yeye vinakuja ndani ya kanisa, kutufanya tujue kwa ufunuo wa Roho Mtakatifu siku gani ambayo tunaishi, kufunua mambo haya makuu, ya ndani, siri zilizofichika [22] (Waefeso 1:15-21; Ufunuo 10:7)

(13) WAKATI WA KUGEUZWA NI SASA

Na Mungu ametuma nguvu zake za kugeuza, Neno lake, ili kukuleta wewe nje ya huu uharibifu wa dini ambao mko ndani yake, mgeuzwe kwa kufanywa wapya nia zenu (Warumi 12:1-2).

Na kuna kitu kimoja tu kiwezacho kuhuisha Neno na huyo ni Roho kwa maana ndiye atoaye – uzima katika Neno. Na wakati uzima ulio katika Neno unapokutana na uzima wa Roho, Unazaa chochote kile mbegu ilicho [23] Na wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu (Warumi 12:2).

Hivyo ndivyo sisi sote tupendavyo kufanya; msiifuatishe namna ya dunia hii, lakini mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu kufanya mapenzi makamilifu yaliyokubalika ya Mungu sasa tumeokolewa, kama tulivyo; sasa tunahitaji nia iliyokuwa ndani ya Kristo iwe ndani yetu, kwamba tunaweza tukageuzwa kutoka mapenzi makamilifu ya Mungu kwa kugeuzwa na Roho kwa Neno lake.

Mambo yale uliyoyawaza kwanza ukayaona ya thamani, weka hayo pembeni na ugeuzwe kwenda kwenye kitu kingine; kwa kile ulichokuwa wakati mmoja, kuwa kile ulicho sasa, unaona? Kwa kufanywa upya nia zenu, kwamba mpate kujua.....lile ambalo ni jema na linalokubalika na mapenzi makamilifu ya Mungu” Oh hilo ndilo tupendalo kujua sisi sote, namna ya kulifanya unaona? Tuko hapa, tunampenda yeye; Ametuokoa sisi, na sasa tunataka kujua litupasalo kufanya. Na tulikuwa tunajaribu kuchukua hatua kidogo kuinuka juu kiasi cha juu kidogo [24].

(14) TUKO KWENYE NJIA YETU TUKIKUWA KWENDA KWENYE UKAMILIFU WA KUFUFUKA, tukiongozwa na Roho. Na sasa tayari umeshafufuliwa. Mungu alipomfufua katika wafu, Alikuina wewe (Waefeso 2:4-6); yule mwana sasa hivi yuko juu yako. Na sasa unakuwa katika maisha ya mafanikio kama alivyokuwa, kufufushwa kikamilifu katika siku za mwisho. Vile utakavyokuwa unavyo sasa. Kwa nini unajua? Nafsi yako imebadilika si ndiyo? Mwili wako umekuja katika utiifu wa hilo, si ndiyo?

Utiifu wa nini? Kanisa? Neno ambalo ni uzima. Sasa wewe umefufuliwa kutoka katika wafu [25] (Wakolosai 3:1-4)

(15) TUNANGOJEA ULE UKAMILIFU WA KUFANYWA WANA, baada ya kupokea Roho wa kufanywa wana [26] (Warumi 8:15) na kwa Roho Mtakatifu tumekuwa mahali petu katika mwili wa Kristo kwa kusudi hapa duniani kuyafanya mapenzi ya Mungu [27] na kutenda kazi pamoja na waliosehemu ya mwili wa Kristo [28]

Ukamilifu wa kufanywa wana utafanyika lini? Wakati wa ufufuko wa kwanza [26] (1 Kor 15:51-54). Sasa ni wakati wa kufanywa wana, Mungu atakapomwaga ukamilifu wake kwetu, Nguvu zake, ufufuo wake, pale ambapo kanisa na kristo tunakuwa karibu sana pamoja mpaka Kristo anaonekana miongoni mwetu, na kufufua wafu na tunaenda kwenye unyakuo [29] (1 Wathes 4:13-18)

(16) BADILIKO LA MWILI: Kinachofuatilia ni mwendo wa haraka (a sweep)Ambao lile kundi dogo litakusanywa pamoja katika mwezi au kama hivyo litakuwa limeondoka (Matayo 27:51-53) mapema tu atakapokuwa wamekusanyika pamoja. Tuko Mwishoni hakuna tumaini lililobakia mahali popote. Mkimbilie Yesu enyi watu! [30] (2 kor 5:1-8; 1 Kor 15:51-54; Wafilipi 3:20-21; 1 Yoha 3:1-3)

(17) KURUDISHIWA (Malak 4:5-6; Yoel 2:23-27)

Kwa maana Mungu alisema, Nitawarudishia yeye anaenda kuwarudishia kwa namna gani? Kwa wajumbe wanne wa mauti waliouuwa huo; halafu kwa wajumbe wanne wa uzima anaenda kuurudisha huo. Wa kwanza alikuwa nani? Martin Luther, kuhesabiwa haki. Wapili alikuwa nani? John WesleyKwa utakaso wa tatu alikuw nani? Pentekoste na kule kurudishwa kwa vipawa, Roho Mtakatifu, ubatizo wa Roho Mtakatifu Wanne alikuwa nani? Lile Neno. Nini? Neno [31]

Ujumbe wa wakati wa mwisho ni kumpata Bibi arusi awe tayari na ajiandae kwa unyakuo. Itafanya nini? Kulingana na

Malaki 4:5-6, ni kuwaleta tena wao kwenye Imani ambayo walikabidhiwa watakatifu mara moja tu (Yuda 1:3) kuwarudisha kwenye Imani ya mababa sehemu ya wapentekoste katika wakati wa kurudishiwa. Nitawarudishia “asema Bwana” Hiyo ni hasa uinjilist wa siku za mwisho [32] kama unataka andiko lingine, chukua hapa, ufunuo 10 na ilisema katika saa wakati wa malaika wa mwisho, malaika wa saba, mjumbe wa saba, atakapoanza kupiga baragumu yake, siri ya Mungu itakuwa imekwisha, kurudishwa tena kwenye Neno Biblia ilisema kwamba mjumbe wa siku za mwisho atawarudisha kwenye imani ya kwanza kwenye Imani ya mababa. Siku za mwisho atarudisha lile Neno la asili (mwanzo) tena kama alivyosema katika Malaki 4 [33] Baada ya kurudishiwa Neno, tunapokea kurudishwa kwa nguvu [34]

(18) AHADI JUU YA KUJA KWAKE kristo ameshaanza kushuka kutoka mbinguni pamoja na Mwaliko, huo ni ujumbe wa kuwaleta watu pamoja, kuwafanya watu tayari (1Wathes 4:15-18) kwanza ni ule ujumbe ukiletwa na kutangazwa, mkate wa uzima ukimleta Bibi Arusi. Pili ni sauti ya ufufuo (kufufuliwa kwa wafu walio ndani ya Kristo) na kitu cha tatu ni tarumbeta, ambayo inawaita watu siku zote kwenye karamu; na hiyo itakuwa karamu ya Bibi Arusi, karamu ya mwanakondoo pamoja na Bibi Arusi huko mbinguni katika mawingu [35].

(19) UASHO:
UAMSHO KWA MAWAZO YANGU, HAUMAANISHI KULETA WASHIRIKA WAPYA. Uamsho sio kundi la waliomgeukia Bwana ingawa haya mambo yanaenda pamoja na uamsho. Lakini uamsho ni kuinua/ kukitia nguvu kile ulicho nacho tayari” kuwafanya wainuliwe/wafufushwe [36] (2 Petro 1:12-15) Bibi Arusi hajapata uamsho bado. Bado hapajawa na uamsho pale
- Hakuna udhihirisho wa Mungu humchemsha Bibi Arusi bado unaona? tunatarajia huo. Itachukuwa ngurumo saba zisizojulikana nyuma pale ili kumuamsha yeye (Bibi Arusi) tena. Atazituma ameahidi hilo. Sasa angalia. Sasa alikuwa amekufa (bibu arusi) [33] (Yohana 5:25 – 27; Waef 2:1-5). Wacha Neno la

Mungu lipewe nafasi ya kwanza. Hicho ndicho tunachohitaji - uamsho! Kuosha kutoamini kote nje na wadudu wote na uzushi na mambo ya kutoa nje na kuona kwamba Mungu bado ni Mungu. Hiyo ndiyo inayotufanya tuwe na uamsho [37].

Ninafikiri huu ni wakati ambao hatupaswi kamwe kuiacha Roho ya uamsho ife. Tunapaswa kuendelea na uamsho, kudumu katika uamsho kila siku. Paulo alisema inabidi afe kila siku ili Kristo aishi (1Kor 15:31) Na hatupaswi kamwe kuachia achia uamsho ufe ndani yetu [38]

Angalia, lakini uone yule Bibi Arusi wa kiroho anapoanza kupata uamsho, anapoanza kurudi na ajiweke mstarini na Neno la Mungu, angalia tena, unaona, jinsi maandiko wakati ule, kutakuwa na ujumbe utakaopita kumpata yule Bibi Arusi – na kumpata yule mwanamke – mteule [39]

Tunasihi uje uamsho wa wenye haki, nguvu nyingi zije miongoni mwetu kanisani kabla tu ya kuondoka kwake. Siyo vigumu kuomba hilo, kwa sababu umeliahidi. Na tunaangalia hilo, Bwana, kwa ule mvuto wa tatu ambao tunajua kwamba utafanya mambo makuu miongoni mwetu na kwa ajili yetu [8]

(20) WAKATI HUU NI WAKATI WA KUWASHA TAA (Matayo 25:6-8)
ujumbe unakuja kwanza sasa “Wakati wa kuwasha taa” Amkeni muwashe taa zenu. Na wakafanya hivyo. Wengine wakaona hawana hata mafuta katika taa zao [35]

(21) WEKA ILE ISHARA (Upendo wa Mungu (Warumi 5:5 Roho Mtakatifu) ! (Matendo 16:31; Kutoka 12:13) Halafu tembea nalo wadai wa nyumbani mwako. Ufanye hivyo sasa. Huu ni wakati wa jioni ni wakati wa kuweka ile ishara sasa! Hasira italeta pigo kati ya siku hizi, na itakuwa umechelewa sasa. Unaona weka Ishara kwa uhakika.

Ishara kwa mwaminio leo ni Roho Mtakatifu, siyo damu. Kemia, lakini ni Roho Mtakatifu wa Mungu . Hivyo ndiyo ishara Mungu

anayoitaka kwa kanisa leo. Mungu lazima aone hii Ishara lazima aione kwa kila mmoja wetu.

Mungu anahitaji ishara kwamba wewe, wewe mwenyewe, umepokea hiyo Ishara yake. Roho Mtakatifu ni njia pekee na ishara pekee ambayo Mungu hawezi ipita kwa sababu ni maisha hasa ya Yesu Kristo yakirudi tena ndani ya mwaminio [40]

(22) UNYAKUO (I Wathes 4:16-17)

Sasa kutakuwepo na unyakuo, tunajua hilo. Hiyo ni siku za mbele [4] neno “kunyakuliwa” – Biblia ilisema “kunyakuliwa juu, kule kunyakuliwa juu” Tunasoma katika 1 Wathesa 4:13-17 ule utaratibu wa kunyakuliwa kule kuku ambako kutafanyika katika siku za mwisho. [35]

(23) ILE KARAMU YA ARUSI YA MWANAKONDOO

MBINGUNI kwa miaka 3^{1/2} (ufunuo 19:6-9)

Sasa kanisa watu wa mataifa litakuwa wapi wakati Yesu akijitambulisha Mwenyewe kwa Ndugu zake? Kumbuka kwamba Bibi Arusi wa Yusufu na wale watoto wawili walikuwa (jumba la kifalme) Ikulu, kwa maana Yusufu aliamrisha kwamba “Hebu kila mtu aondoke; wawekeneni wote mbali na mimi “(Mwanzo 45:1-5) Kwa hiyo Bibi Arusi wa mataifa alikuwa amefichwa kwenye jumba la kifalme (Ikulu) la Yusufu. Kanisa la Mataifa litaenda wapi kwenye unyakuo? Litakuwa kwenye jumba la kifalme (Ikulu). Bibi Arusi ataondolewa kutoka duniani atakuwa amenyakuliwa juu kabla ya dhiki ile kuu kukutana na Bwana wake mawinguni. Kwa miaka mitatu na nusu wakati wa hasira ya Mungu inamwagwa (Ufunuo 11:1-6); Daniel 12:1) atakuwa kwenye karamu kuu ya Arusi ya mwanakondoo. Halafu atarudi, na kumuacha Bibi Arusi wake “Nyumbani kwa Baba yake”, (Yohana 14:1-3) wakati anajifunua mwenyewe kwa ndugu zake. Wakati huu hasa, lile Agano la mpinga Kristo ambalo wayahudi wameweka na Roma litavunjwa. Rumi na washirika wake watapeleka majeshi yao kuungamiza wote wanao mcha Mungu Wayahudi wanaoshika Neno (Zakaria 12:1-14;13:6).

Lakini wanapokuja kinyume na huo mji ili kuuangamiza, kutakua ishara mbinguni ya kuja kwa Mwana wa Adamu na Majeshi yake kuwaangamiza wale walikuwa wakiiharibu dunia (Matayo 24:29-31)

maadui watakapofukuzwa. Yesu anakuja na kujionyesha mwenyewe kwa wale 144,000. Kwa kuwa wameuona mkono wake wa wokovu, wamekuja kuzijua nguvu zake. Lakini sasa wanapooni makovu yake na wanajua walimkataa yeye hata wakati ule itawafanya walie/waomboleze kwa kuugua sana na kwa uongo, kama walivyofanya ndugu zao zamani waliposimama mbele ya Yusufu wakiogopa kwamba wanaweza wakauawa lakini kama Yusufu alivyosema, “Msihuzunike, wala msiudhike nafsi zenu, ni sawa tu. Mungu alikuwa katika jambo hilo lote. Alifanya hilo kuhifadhi uhai “Kadhalika Yesu atazungumza nao amani na upendo (42) mpende, mpende mpende yeye! Ona yale aliyokufanyia wewe ni kwa upendo; upendo unaleta utiifu; upendo unaleta ubembelezio (uchumba); upendo unaleta ndoa; hapo ndipo tunapokwenda; kwenye karamu ya arusi ya mwanakondoo. Ninamsikia mwokozi wangu anaiita kwamba ananipenda mimi pia (40).

24) TUKO KATIKA KUTOKA KWA TATU. Mungu sasa anaita kutika kwa kiroho kutoka Babyroni ya kiroho kuja kuwa mteule wake ni kwa wateule wake tu. Ile nguzo ya moto, upako ule ule wa Roho ukiongoza kwenye nchi ambayo amehidi kwetu sisi. Sasa anawatoa kutoka ubatizo wa kiroho (1 Kor 12:13) wa Roho Mtakatifu kuwaleta tena katika nchi ya milele ya utawala wa miaka elfu (1 saya 65:17-25: Isaya 25:6-8) na mambo makuu baada ya hapo (43)

25) YEYE ASHINDAYE, NITAMPA KUKETI PAMOJA NAMI KATIKA KITI CHANGU CHA ENZI (kwenye ufalme wangu) – wakamiliki na kutawala pamoja na Mfalme Mkuu katika Mileniam, utawala wa miaka 1000 ya amani (ufunuo 3:20 – 21: ufunuo 20:4-6) Ni baraka ya ajabu sana kumjua Bwana Yesu kama mwokozi wetu, na kumjua yeye kama mponyaji wetu, na kumwangalia yeye kuja kama mfalme wetu ili asimamishe ufalme wake hapa duniani, kwamba tutatawala na kumimiliki pamoja naye kwa miaka elfu, kuwa naye milele (44) (Isaya 32:1-2). Hebu maisha yetu yawe tamesalimishwa kwake kiasi kwamba Roho Mtakatifu ataishi mwenyewe kupitia sisi na kuzungumza kupitia sisi, Bwana. Hebu tukumbuke akilini mwetu kadiri tunavyotembea barabarani na kuchuana na mikono yetu na dunia, na mahali pao sahihi hapa duniani. Tutachukuwa nafasi ya nyuma, tukijua kutawala, Bwana. Na ufalme wetu mkuu karibu utatokea na kuchukua falme zote ambazo ziko katika miliki yake, na

washindi watatawala na kumiliki pamoja naye hapa duniani kwa miaka elfu na kuwa naye milele. (45).

Nukuu za Kiingereza

- [1] Mtazame Yesu (63-1229), uk 31
- [2] Kuthibitisha neno lake (64-0816) Aya 236
- [3] Mungu mkuu akifunuliwa mbele yatu uk 21 – 22
- [4] Wapakwa mafuta wa wakati wa mwisho Aya 269
- [5] kutaharuki (963-0901) Aya 21
- [6] karamu ya baraguni (640719M) Aya 243
- [7] maono ni nini (56-0408A), uk 18
- [8] shitaka (63-0707), uk 62
- [9] mtazame Yesu, Uk 7
- [10] maswali na majibu (64-0823m) uk 955
- [11] imani kamilifu (63-0825E) Aya 184
- [12] kutaharuki Aya 22-23
- [13] Mungu mkuu akifunuliwa mbele yetu uk 15
- [14] “kufunuliwa kwa Mungu” (64-0614m)
- [15] nini kinavutia kule mlimani Aya 119
- [16] kristo ni siri ya Mungu iliyofunuliwa kwa Mungu” (63-0728), uk 83-85
- [17] Nimfanyieje Yesu aitwaye (64-1124m) Aya 115-116
- [18] waaminio wa aina tatu uk 15
- [19] ni kuchomoza kwa jua uk 15
- [20] muhuri wa kwanza, uk 128, 142
- [21] kanisalaodikia KCNS uk 327
- [22] wiki 70 za Daniel Aya 67
- [23] nguvu za Mungu za kugeuza Aya 243 – 244 212-213
- [24] “Nguvu ya kugeuza” Aya 39,45-48
- [25] “Ni kuchomoza kwa jua” uk 50-51, 29
- [26] Ufunuo 5 Nyoka aliyejeruhiwa Aya 108
- [27] shujaa mkuu david Aya 28,32
- [28] Bwana atajipatia (57-0326), Aya 85
- [29] “kwa nini tumepewa Roho Mtakatifu” Aya 51
- [30] kutoa presha (62-0518), Aya 112
- [31] kurudishiwa kwa mti wa Bibi Arusi uk 75
- [32] uinjilist wasiku za mwisho Aya 222
- [33] muhuri watatu, uk 252-253

- [34] Beana atajipatia (64-0402) Aya 61
- [35] kunyakuliwa Aya 128, 130, 141, 152 – 154
- [36] Israel kule misri Aya 1
- [37] uwepo wa Mungu usiotambulika, Aya 4-5
- [38] Nitawezaje kushinda Aya 33
- [39] “muungano usioonekana” uk 8
- [40] ile ishara (63-0901), uk 10 49-50, 59-60
- [41] “Mambo yatokavyokuwa”, Aya 20
- [42] “ufunuo wa Yesu Kristo”, KCNS UK 40
- [43] kutoka kwa tatu, uk 37, 45
- [44] usiogope ni mimi (60-0305), Aya 20
- [45] Paulo mfungwa wa Yesu Kristo uk 2

Jiwe la kiroho la kujengea na. 152 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, Yamekusanywa na Gerd Rodewald friedenstr. 69 D-75328 Schomberge, Germany Simu (+49) 72357613 Fax (+49) 72353306

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia na mbegu zitaingia gazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia. Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)

Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:

*Charles E.Y. Kanju
Box 5138, Tanga
E-mail: chaelika@Hotmail.com
cellphone: 0784 704299*